

# MAOMBI

**Ya  
Kujikuza  
kiroho**

TOLEO LA 6



BY DENIS & DEVIS JULIUS

## **MAOMBI MAALUMU YA KUJIKUZA KIROHO.**

### **UTANGULIZI:**

Nakukaribisha katika mfululizo wa mwongozo wa kimaombi, unaohusiana na eneo letu la ukuaji kiroho. Kumkaribia kwetu Mungu kunategemea sana kiwango chetu cha ukuaji kiroho. Ulishawahi kujiuliza kwanini Mungu ajitambulisha kama “mzee wa siku” (Danieli 7:9), Au wale wazee ishirini na wanne (24wanaokizunguka kiti cha enzi kule mbinguni waitwe “wazee”? Sio kwasababu sura zao ni za kizee, hapana Ni kwasababu rohoni ni wakomavu wa kutosha mfano wa wazee. Na ndio Maana wakawa karibu na Mungu kwasababu Mungu naye ndivyo alivyo. Na sisi pia tunapaswa tuongeze bidii tukue katika eneo hili. Tusibakie kuwa wachanga tu sikuzote.

Usikubali kuwa mkristo asiyepiga hatua, kiwango chako cha mwaka jana kiwe tofauti na cha mwaka huu, Vilevile kiwango chako cha kujifunza Neno mwezi uliopitai kisiwe sawa na mwezi huu.

Kumbuka ukuaji haategemei sana wingi wa miaka uliyokaa kwenye ukristo halafu hujishughulishi na lolote, unategemea na bidii na juhudu unazotia katika kuyatenda mapenzi ya Mungu kwa wakati ulionao.

Hivyo katika makala hizi, tunaangazia hususani Eneo la maombi, lakini pia yapo mafundisho mbalimbali yatakayokusaidia upige hatua hizo kwa haraka, fungua tovuti yetu hii [www.wingulamashahidi.org](http://www.wingulamashahidi.org). Na huko takutana na mafundisho zaidi ya elfu nne (4,000), ikiwemo maswali mengi ya biblia yaliyojibiwa. Ukichanganya Neno na Maombi ndivyo ukuaji wako unavyokuja rafiki.

Maombi haya ni ya SAA SITA (6), kwa wiki, unaeweza kuombea kipengele kimoja kwa siku, au viwili au vitatu n.k. mpaka utakapomaliza wiki unakuwa umekalimilisha saa zote sita na vipengele vyake vyote. Na utakuwa umeongeza kitu ndani mwako kuliko ungekaa tu bila kuomba.

# UTAKASO WA ROHO, NAFSI, NA MWILI

## ~Toleo la 6

*1Wathesalonike 5:23 Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi **nafsi zenu na roho zenu na miili yenu** mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo.*

Hapo, yanatuonyesha kuwa Roho zetu, Nafsi, na miili vinapaswa vitakaswe na Mungu Tunatakaswa kwa Neno, lakini pia kwa maombi. Tunapojiombea ndivyo tunavyojengwa. Hivyo hatuna budi kujiombea sehemu hizo kuu tatu zinazotukamilisha sisi wanadamu.

### 1. ROHO (saa 2)

Roho ni chumba cha ndani kabisa cha mtu.

Ni mahali pekee ambapo **IBADA** yoyote ya mwanadamu inaanzia. Ibada haitoki kwenye nafsi au kwenye mwili, bali rohoni. Hivyo roho ikichafuka, ibada huchafuka.

Yohana 4:23 Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu.

Kama Roho yako imetakasika vizuri utajikuta vitu hivi vinatoka ndani yako;

- utaifurahia Ibada kwa Mungu, na itatoka ndani.
- Unafurahia maombi
- Unakuu na hamu ya kusoma Neno la Mungu wakati wote
- Unapenda sana kwenda nyumbani (Kanisani) kwa Bwana kama Daudi alivyosema nalifurahia waliponiambia twenda nyumbani mwa Bwana.
- Unakuwa na Shauku ya kuwashuhudia wengine habari njema.
- Unakuwa mwepesi kumsikia au kumwelewa Mungu anaposema na wewe kwa njia zake.
- Utachukia ibada zote za sanamu: Kumbuka sanamu sio tu kile kinyago kilichochoywa na watu kuvisujudia hapana, bali kwetu sisi tuliozaliwa katika agano jipya ni zaidi ya hivyo, bali ni pamoja na kupenda mambo yoyote yale ya kidunia zaidi ya kumpenda Mungu, mfano mpira, pesa, mali n.k. hivyo ni masanamu.

Hivyo kama mtu unayetaka kuwa afya rohani, huna budi kumwomba Bwana akutengeneze katika maeneo yafuatayao ndani ya roho yako;

- ✓ Bwana akupe **Nguvu za rohani**: Ikiwa na maana Kuomba na kukesha
- ✓ Bwana akupe **wepesi wa rohani**: Wa Kusikia sauti ya Mungu na kutii
- ✓ Bwana akupe **Ulinzi wa rohani** > Usivamiwe na mapepo/ roho zidanganyazo, zikakufanya utoke nje ya imani.
- ✓ Bwana akupe **Afya rohani**: Kushibishwa vema na Neno la kweli la Mungu
- ✓ Bwana akuishe Mavazi ya rohani: Upende Utakatifu, usiende uchi (Ufunuo 16:15)
- ✓ Akupe **Utulivu rohani**: Yaani uwezo wa Kuzingatia vitu vya Ki Mungu na kutafakari. Makelele yasiwepo.
- ✓ Bwana aijenge **Madhabahu yake rohani**: Bwana aijenge vema kambi yake ndani yako, ambayo haijaundwa kibinadamu bali na Roho wa Mungu.

**Zingatia**: Hakikisha katika kuomba kwako unaomba kwa kujimimina, Roho Mtakatifu atakusaidia kukupa maneno mengine ya kuombea kuhusiana na eneo hili la roho yako.

## 2. NAFSI (saa 2)

Tofauti na roho ambapo panatoka ibada, Katika nafsi ndipo zilipo hisia, na tabia zote zote za mtu,. Nafsi ya mtu ikijengeka vizuri, ndio panatoka Upendo, Amani, utu wema, furaha, fadhili, upole, uvumilivu, huruma n.k. Lakini nafsi ya mtu ikiharibika, kunatoka mambo mabaya.. kama vile ukorofi, wivu, fitina, hasira, kiburi, usengenyaji, matusi, tamaa, mawazo mabaya, uongo, Pamoja na woga, hofu, mashaka, huzuni, na uasherati.

Bwana Yesu alisema...

*Mathayo 15:18 Bali vitokavyo kinywani vyatoka moyoni; navyo ndivyo vimtiavyo mtu unajisi. 19 Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati; wivi, ushuhuda wa uongo, na matukano;*

Kumbuka nafsi ya mtu inatafsirika pia kama moyo (Marko 2:8).

Hivyo ni huna kuombea kwa bidii maeneo haya muhimu katika nafsi yako ili ujengwe.

- ✓ **Kiasi**: Mipaka katika kutenda kila jambo ambalo halihusiani na ibada. Bwana akujalie kiasi,
- ✓ **Uvumilivu**: Bwana aijenge nafsi yako, aiondoe pupa akupe uvumilivu na subira

- ✓ **Fikra za moyoni:** Bwana atakase fikra zako, usiwaze maovu, mawazo yako yasafike kila wakati.(Mwanzo 6:5)
- ✓ **Usafi:** matusi, masengenyo, , tamaa, kiburi, majivuno, visizalike ndani yako
- ✓ **Ujasiri:** Bwana akuondolee kumwonea yeye haya, au injili yake. Uwe jasiri. Katika wokovu wako kwa ulimwengu.
- ✓ **Furaha:** Furaha ni jambo la muhimu sana katika afya ya nafsi yako, Mungu aijenge na kukuzidishia furaha yake na raha yake nafsini mwako.(Mathayo 11:29)
- ✓ **Kujitoa:** Bwana akupe moyo wa kujitoa kwa ajili ya wengine, na injili yake. Kama Bwana na mitume wake walivyojitoa nafsi zao, kiasi hata cha kutoa uhai wao kwa wengine. Ndivyo na wewe unapaswa uwe, kwasababu hicho ndio kielelezo cha Upendo.
- ✓ **Uthabiti:** Bwana akupe uthabiti wa moyo. Usizimie kiwepesi, upishanapo na majaribu au upitapo jangwani. Imani yako izidi kuimarisha
- ✓ **Ulaini:** Ugumu wa moyo/nafsi hupelekea Bwana kutosema na wewe, moyo wa jiwe humfanya Mungu asiwe karibu na mtu. Hivyo omba Bwana aifanye moyo wako kuwa mlaini, sikuzote akuagizapo, uwe mwepesi kutii.
- ✓ **Hazina:** Moyoni ndipo panapohifadhiwa kila aina ya taarifa, na mawazo, hivyo hazina yako ikijaa mambo maovu ya kidunia, kitakachotoka kitakuwa hicho hicho, lakini kukijaa mambo masafi na mema, ndiyo yatakayotoka. Mwambie Bwana nipe kuchuja, kinachoingia kwenye hazina yangu.

**Cha ziada:** Ujaliwapo pia kuomba kwa lugha, pia ni vema, kwasababu husaidia kujijenga nafsi yako zaidi.

*1Wakorintho 14:4 Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake; bali ahutubuye hulijenga kanisa.*

### 3. MWILI (saa 2)

Mwili ndio nyumba ya Roho yako na nafsi yako. Lakini cha ajabu ni kwamba sio nyumba yako tu peke yake bali ni pamoja na ya Mungu.

*1Wakorintho 3:16 Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? 17 Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.*

Hivyo mwili ukiharibika, au usipotunzwa, utaathiri makao yako wewe na yale ya Mungu pia

Hivyo kama ni nyumba ya Mungu haina budi kuheshimiwa. Na kutunzwa. Kwasababu ukiwa na afya na nguvu na heshima, Mungu atapata nafasi bora ya kutembea katika nyuma yake nzuri. Lakini ukaanza kujichubua, kuva uchi uchi, kuweka winyoyo ya kipagani kichwani, kujiwekea marangi usoni, kujibadili jinsia, kuzini, n.k. unatafuta kifo.

Ombea maeneo haya muhimu katika mwili wako.

- ✓ **Afya:** Afya njema, hukufanya uweze kuomba, kwenda ibadani, kwenda kuhubiri, lakini ukiwa mgonjwa kitandani, au umepooza upande mmoja wa mwili utawezaje, kumtumikia Bwana. Hivyo ni kuomba daima Bwana akupe afya hata kama leo ni mzima, omba ulinzi kwa ajili ya siku zijazo, Bwana akuepushe na magonjwa, maajali, madhaifu n.k.
- ✓ **Hisia:** Bwana akupe nguvu ya kuzitawala hisia zako za mwili. Hapa ndipo watu wengi wanaposhindwa, na kujikuta wanaangukia katika uzinzi na uasherati.

*Wimbo ulio bora 2:7 Nawasih, enyi binti za Yerusalemu, Kwa paa na kwa ayala wa porini, Msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, Hata yatakapoona vema yenyewe*

Uzinzi na uasherati ni dhambi moja inayomfukuzia mbali Roho Mtakatifu ndani yako, kwasababu unaifanya katika mwili wako mwenyewe. Omba kisha chukua hatua za kuweka mbali vichocheo vya kizinzi, kwasababu moto hufa kwa kukosa kuni.

- ✓ **Starehe:** Mwombe Bwana akusaidie, uushinde mwili katika eneo la starehe. Starehe ni pamoja na vyakula, na vinywaji. Ukiwa ni mlaji sana, kila wakati unaupa mwili chakula kila utakapo, huwezi kufunga, utapata hasara, kiroho utakuwa chini, Ikiwa kila wakati unaupa mwili usingizi unaona uvivu kusali, utapata hasara. Ikiwa huwezi kuvumilia kukaa uweponi mwa Bwana masaa mengi, unajiona uchovu na wewe unautii mwili, kamwe kumkaribia Mungu itakuwa ni vigumu kwako.

Paulo alisema;

*1Wakorintho 9:27 bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.*

- ✓ **Macho:** Macho ni mlango mwingine unaweza kuujenga, au kuuathiri mwili kwa sehemu kubwa. Yesu alisema.

*Mathayo 6:22 Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru. 23 Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo!*

Bwana akupe uzito, wa kutotazama kila kitu upishanacho njiani, au mitandaoni, au kazini au popote. Kama vile Ayubu alivyosema nalifanya agano na macho yangu. Macho yako uwe makini nayo.

- ✓ **Mavazi na mwenekano:** Roho Mtakatifu ashuhudie ni nguo ipi yenye kukufaa, yenye utukufu kwake. Ambapo halitakuwa kwazo kwako wewe, wala kwa wengine. Yapo mavazi utayaona ni mazuri lakini Bwana ameyakataa kwako. Tukiachilia mbali yale ya kidunia na ya kizinzi. Hivyo Bwana akupe uchaguzi wa mavazi, watu wakikuona wafahamu kweli Yule ni mwana wa Mungu. Itakuongezea kibali kizuri mbele za Mungu.

Kwa hitimisho ni kuwa ukizingatia kuombea maeneo hayo matatu muhimu yaani Roho, Nafsi, Mwili, Basi Bwana atakutakasa, na hivyo utanza kuona wepesi wa kiroho na kimwili uwapo mbele zake. Kumbuka sote tuna wajibu wa kukua kiroho, tupige hatua nyingine ya juu katika Bwana ili tufikie kile kimo cha ukamilifu wa Yesu Kristo.

Ukizingatia kuomba SAA MBILI (2), kila eneo ndani ya wiki moja, Yaani saa 2 roho, saa 2 nafsi, na saa 2 mwili. basi utakuwa umejiimarisha pakubwa sana. Na utanza kuona mabadiliko.

Tenga muda wako wa utulivu kila siku wa kuomba.

Bwana akubariki.

Mwendelezo mwingine unakuja..

Kwa ushauri/ Msaada/ Maombezi wasiliana nasi kwa mawasilino haya;

Na, Mwl Denis & Devis Julius  
Nuru\_ya\_Upendo  
Website: [www.wingulamashahidi.org](http://www.wingulamashahidi.org)  
Email: [info@wingulamashahidi.org](mailto:info@wingulamashahidi.org)  
+255693036618/ +255789001312